# Kuhusu Mwongozo Huu

1.1 Hadhara lengwa ya mwongozo huu 9

1.2 Kwa nini tunahitaji mwongozo huu 9

1.3 Jinsi mwongozo huo ulivyobuniwa 10

1.4 Hadhi ya mwongozo huu 11

1.5 Marejeo 11

MAHARAGWE YA KIFARANSA, MITABU CHA MICHA, PICHA NA.8

# Kuhusu Mwongozo Huu

**Mwongozo huu unatoa mashauri na zana za Kufanyia kazi zilizopendekezwa na kundi la mradi wa wakulima wadogo wa ETI kwa ajili ya wale wanaofanya kazi katika mtungo wa ugavi wa bidhaa zitokazo kwa wakulima wadogo. Mwongozo wenyewe unalenga kutoa ushauri wa jinsi wauzaji wa rejareja, wanunuzi, wakulima wadogo na wengineo wanaweza kuchukua hatua za kuboresha kazi ya wakulima wadogo. Lengo kuu ni kujaribu kufikia utekelezaji wa viwango vinavyokubalika kimataifa kuhusu ukulima mdogo, na hasa, vile vya mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI.**

## 1.1 Hadhara lengwa ya mwongozo huu

Mwongozo huu unakusudiwa kutumiwa na makundi mbalimbali yanayohusika na mtungo wa kimataifa wa ugavi wa bidhaa zinazotoka kwa wakulima wadogo. Kimsingi, mwongozo huu unalenga wahusika wa biashara muhimu kwa mitungo hii ya ugavi. Vilevile unasheheni sehemu za kutumiwa na makundi yasiyo ya kibiashara, kama vile vyama vya wafanya kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohusika katika uboreshaji wa viwango vya kazi kwenye uwanja huu. Mwongozo huu uliasisiwa na wanachama wa ETI, hasa kwa ajili ya wanachama wengine, lakini pia unalengwa kufaidi sehemu kubwa kati ya wasio wanachama, hasa:

- Wauzaji rejareja
- Wanunuzi ikiwa ni pamoja na wakala, vyama vya ushirika, wauzaji bidhaa nje, makampuni ya kufunga bidhaa katika vifurushi, na wagawaji
- Wakaguzi wa mahesaba wa kibiashara wanaohusika katika kukagua wakulima wadogo au wanunuzi
- Wakulima wadogo
- Vyama vya wafanya kazi
- Mashirika yasiyo ya kiserikali

Vilevile mwongozo huu utawavutia wanataaluma wanaoshughulikia masuala ya ukulima mdogo.

## 1.2 Kwa nini tunahitaji mwongozo huu

Utumiaji wa mfumo wa kanuni za kazi kwa wazalishaji wadogo wa kilimo ni suala muhimu na lenye utata miongoni mwa wauzaji rejareja na wanunuzi pamoja na vyama vya wafanya kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohusika na shughuli za haki za wafanya kazi. Utafiti na tajriba za wanachama umeonyesha kuwa wakulima wadogo na wafanya kazi wao huwa mara kwa mara wanajipata katika masharti maghumu na na hali duni kikazi.

Wakati huohuo, wakulima wadogo wanaonekana wanaongezeka katika mitungo ya kimataifa ya ugavi ya wanachama wa ETI. Kiwango ambacho masoko hutegemea bidhaa kutoka mashamba madogo kinatofautiana kulingana na bidhaa, lakini kwa bidhaa zingine, kama vile, kahawa, wakulima wadogo ndio wanaokuza kiasi kikubwa zaidi kinachouzwa katika masoko ya ulimwengu. Katika nchi nyingi zinazoendelea, mashamba madogo ndiyo kitengo cha kikuu cha uzalishaji wa kilimo.

Hata hivyo, licha ya umuhimu wao katika mitungo ya ugavi, wakulima wadogo wanatoa changamoto mbalimbali kwa wauzaji rejareja na wanunuzi waliojitolea kutekeleza kanuni za kazi. Changa moto hizi ni pamoja na:

- Idadi na uwezekano wa kupatikana kwa wazalishaji wadogo zaidi wanaohusika;
- Gharama za kusimamia idadi kubwa ya wazalishaji waliotawanyika;
- Matatizo ya kutambua na kuainisha wakulima wadogo, yanayotokana na fasili tofautitofauti za mashamba madogo na taratibuambazo zitatumika kuunganisha wakulima wadogo na mitungo ya kimataifa ya ugavi wa bidhaa;
- Umbali wa wauzaji rejereja kutoka kwa mkulima mdogo, unaosababishwa na urefu na utata wa mitungo wa ugavi unaowaunganisha;
- Uhaja ya kufasili jinsi kanuni zenye msingi katika viwango vya kimataifa vya kazi, zilizobuniwa hasa kuimarisha mahali pa kufanyia kazi kuambatana na hali za kikazi zisizo rasmi, kwa mfano ukulima katika mashamba madogo.

Kwa hivyo, kuna haja kubwa ya ushauri maalum na vilevile zana za kazi za kutumiwa na wale wanaohusika katika nyanja mbalimbali za mitungo ya ugavi ili kuwawezesha wote kuboresha hali za kikazi za wakulima wadogo. Mwongozo huu unanuia kutoa msaada huo.

## 1.3 Jinsi mwongozo huo ulivyobuniwa

Mwongozo huu ulitengenezwa na kundi la mradi wa wakulima wadogo wa ETI katika kipindi cha miaka mitatu, 2002 -2004. Kundi hili linajumuisha vijikundi vitatu, yakiwemo makampuni, wawakilishi wa vyama vya wafanya kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Makampuni katika kundi hili ni pamoja na wauzaji rejareja kutoka sekta ya vyakula na bidhaa zingine na pia wauzaji wakubwa na wadogo walio na uzoevu wa kununua aina tofautitofauti za bidhaa kutoka kwa wakulima wadogo wakitumia taratibu mbalimbali za ununuzi. Kundi zima lina uzoevu mkubwa wa kiutendaji wa kufanya kazi na wakulima wadogo wadogo au kwa ajili yao.

Kundi hili kwanza liliagiza kutekelezwe utafiti wa kutathmini maarifa na tajriba ya wanachama wa ETI kuhusu wakulima wadogo waliomo katika mitungo ya ugavi. Kufuatia utafiti huo, kundi hili lilifafanua malengo ya mradi ambayo ni:

- Kugundua jinsi mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI unavyotumika kati ya wakulima wadogo na jinsi unavyoweza kutekelezwa na kusimamiwa na wakulima wadogo pamoja na wafanya kazi wao;
- Kuibua mbinu za kufanya kazi na wakulima wadogo pamoja na wafanya kazi wao ili kuendeleza uwezo wao wa kufuata kanuni huku wakitambua kwamba mbinu moja haitafaa kila nchi, zao au mkulima mdogo;
- Kuandika mitazamo mbalimbali ya utekelezaji wa kanuni hizo katika miundotofauti tofauti ya mtungo wa ugavi.

Ili kuyafikia malengo haya, kundi hili lilifanya shughuli mbalimbali. Hizi zilikuwa ni pamoja na kukusanya habari za kazi za wanachama kuhusu eneo hili hadi leo; kufafanua jinsi mfumo wa kimsingi wa kanuni za ETI unatumika kwa wakulima wadogo kukubaliana juu ya mtazamo wa ETI. Kundi hili pia lilikubaliana kuwepo kwa haja ya kisa na nchi ya kufanyia utafiti ambapo tunaweza kujifunza kutoka kwa mitazamo ambayo tayari inatumika na kutafuta ushauri kuhusu mbinu za ETI zilizopendekezwa za kutumia, kutekeleza na kusimamia viwango vya kazi pamoja na wakulima wadogo.

Mwongozo huu, uliondikwa kwanza na kundi hili mnamo mwaka wa 2002 -2003, umepitia masahihisho matatu muhimu.

- Sahihisho kuu la kwanza lilifuatia mashauriano na makundi ya washikadau walio katika shughuli za chai na mazao mabichi nchini Kenya. Washikadau walioshiriki walikuwa ni pamoja na wauzaji rejareja, wanunuzi, maafisa wa serikali, wawakilishi wa vyama vya wafanya kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Utaratibu huo wa mashauriano ulituwezesha kutambua mianya ya maarifa ambayo ilitupelekea kufanya utafiti pamoja na wakulima wadogo na wafanyakazi wao nchini Kenya. Sahihisho kuu la pili lilitilia maanani matokeo ya utafiti huo.
- Matokeo ya utafiti yalipatiwa washikadau wa Kenya mnamo Novemba 2004, na majibu yao yakatiliwa maanani katika sahihisho la tatu.

## 1.4 Hadhi ya mwongozo huu

Mwongozo huu ni kipengee cha jukumu linaloendelea. Wanachama wa kampuni ya kundi hili wananiua kuutumikisha mwongozo huu katika mitungo yao ya ugavi wa mazao tofautitofauti katika nchi mbalimbali. Matumaini yetu ni kutumia mafunzo yatakayopatikana kusahihisha mwongozo huu na kutayarisha toleo la pili hapo mwaka wa 2006. Utafiti kuhusu Kenya unaorejelewa hapo juu, umechangia kubuni mwongozo huu. Yatupasa kutaja kuwa mwongozo huu umeandikwa kwa ujumla. Kwa hivyo, utahitaji kubadilishwa na watumiaji tofautitofauti ili uyafae mahitaji yao mbalimbali.

## 1.5 Marejeo

Mwongozo huu umeandikwa kwa kurejelea nyaraka zifuatazo:


Mikutano na mashauri ya Shirika la kimataifa la wafanya kazi: mkutano wa 138 wenye mada *Minimum age for admission to employment*, na mapendekezo yake yanayoambatana ya 146; mkutano wa 182 wenye mada *Worst forms of child labour*, na mapendekezo ya 190; mkutano wa 184 na mapaendekezo ya 192 yenye mada *Safety and health in agriculture*

Oxfam, *Fair Trade Programme: policies and procedures manual*, Januari 2001

Natural Resources Institute, *Smallholders in export horticulture: a guide to best practise*, NRI, Chuo Kikuu cha Greenwich, 2002

Natural Resources and Ethical Trade Programme, *Theme Paper 6: Managing codes in the smallholders' sector*, NRI, 2001

Fairtrade Labelling Organisations International, *Generic fairtrade standards for small farmers* organizations/hired labour, 2001

The Europe African Caribean Pacific Liason Committee (coleacp), *Harmonised framework, 2000*. Hii inawasilisha uwiano wa kanuni za kiutendaji za vyama kadha vya biashara ya nje ya mboga na matunda katika Afrika Mashariki na kusini

Convention on the Elimination of all forms of Discrimination against Women (CEDAW) Article 11, 1979

UN Fourth World Conference on Women, *Platform for action, Chapter 5*, 1995

Wine Industry Ethical Trade Association, *Manual for members of the Wine Industry Ethical Trade Association*,

WIETA, South Africa, 2003

Agricultural Ethics Assurance Association of Zimbabwe, *Participatory social auditing of labour standards: a handbook for code of practise implementaters*, AEAAZ, 2002

International Labour Organisation Bureau for Workers' Activities, *Bitter harvest: child labour in agriculture', 2002.*

International Labour Organisation, Multinational Enterprises Programme, in focus programme on strengthening social dialogue, *Nation I tripartite seminar on the Triapartite Declaration of Principles concerning Multinatjonal Enterprises and Social policy, and social dialogue in the plantation sector in Kenya: report on proceedings, 2002.*